HALMASHAURI YA WILAYA YA KYELA

TAARIFA YA MAENDELEO YA ELIMU YA MSINGI MWAKA 2021 ILIYOSOMWA KATIKA KIKAO CHA WADAU WA ELIMU KILICHOFANYIKA TAREHE 15.6.2022

1.0. UTANGULIZI

Kwa mwaka 2021, Halmashauri ya Wilaya ya Kyela ilikuwa na jumla ya Shule za Msingi **107** zikiwemo **102** za Serikali na zisizo za Serikali **5**. Aidha, shule za Msingi zote zilikuwa na Madarasa ya Awali.

Jedwali Na. 1: Taasisi za Elimu ya Msingi

Tarafa	Shule za Awali	Shule za Msingi		
		za serikali	zisizo za serikali	Jml
Unyakyusa	56	53	3	56
Ntebela	51	49	2	51
Jumla	**107**	**102**	**5**	**107**

2.0 HALI YA ELIMU YA MSINGI

2.1 Elimu ya Msingi

Kwa Mwaka, 2021 Halmashauri ilikuwa na jumla ya wanafunzi **49,319** (wav **24,846** na was. **24,473**) wa Darasa la Awali hadi la Saba wakiwemo wanafunzi **389** (wav. **174** na was.**215)** wa Shule zisizo za Serikali. Aidha, kati yao Wanafunzi **7,402** (wav.**3759** na was.**3643**) walikuwa wa Madarasa ya Awali.

2.1.1 Uandikishaji wa Darasa la Awali na Darasa la Kwanza 2021

2.1.1.1 Elimu ya Awali

Mwaka 2021, Halmashauri ilikuwa na Madarasa ya Elimu ya Awali **107** katika Shule zote za Msingi **107**. Hadi tarehe **31 Machi 2021,** Halmashauri ilikuwa imeandikisha jumla ya watoto **6,196** katika Shule za serikali wakiwemo wavulana **3,161** na wasichana **3,035** sawa na **101.4%** ya wanafunzi **6,111** (wav **3,052** na was.**3,059**) waliotarajiwa kuandikishwa kipindi hicho. Hali hiyo ilipelekea kuvuka lengo kwa **asilimia 1.4.** Aidha,

jumla ya watoto **111** (wav**.59** na was**.52)** sawa na **85.4%** ya watoto **130** (wav**.63** na was**.67)** ya waliotegemewa waliandikishwa katika Shule zisizo za Serikali.

2.1.1.2 Darasa la Kwanza

Hadi tarehe 31 Machi 2021, Halmashauri ya Wilaya ya Kyela ilikuwa imeandikisha jumla ya wanafunzi **7,123** (wav**.3,582** na was**.3,541)** wa Darasa la Kwanza sawa **111.0%** ya wanafunzi **6,394 (**wv. **3242** was.**3,152)** waliotarajiwa kuandikishwa. Pia jumla ya watoto **97** (wav**.46** was**.51)** sawa na **113%** ya watoto **86 (**wav**.42** na was**.44)** waliotarajiwa waliandikishwa katika Shule zisizo za Serikali.

Kwa mwaka 2022, Halmashauri ilitarajia kuandikisha jumla ya wanafunzi **6,688** wa Darasa la Awali wakiwemo wavulana **3,311** na Wasichana **3,377.** Kwa upande wa Darasa la Kwanza matarajio yalikuwa kuandikisha Wanafunzi **6,771**(wav.**3,406** na was.**3,365**). **Hadi tarehe 31 machi 2022**, jumla ya wanafunzi **7,144** (wav.**3,706** na was.**3,438**) sawa na **106.3%** walikuwa wameandikishwa Darasa la Awali na **7,393** (wav.**3,741** na was.**3,652**) sawa na **109.2%** walikuwa wameandikishwa Darasa la Kwanza.

2.1.2 Hali ya Miundombinu na Samani katika Shule za Msingi

Kwa mwaka 2021, Halmashauri ya Wilaya ya Kyela ilikuwa inahitaji jumla ya vyumba vya madarasa **1,565** kwa ajili ya wanafunzi wa Shule za Msingi za Serikali. Vyumba vilivyokuwepo **992** hivyo kufanya upungufu kuwa vyumba **580** sawa na **37%.** Mahitaji ya madawati ilikuwa **19,355** yaliyokuwepo **16,599** kufanya upungufu kuwa madawati **3,553** sawa na **18.4%.**

Halmashauri ilikuwa na jumla ya matundu ya vyoo **1,385** kati **2,256** ya yaliyokuwa yanahitajika na kufanya upungufu wa matundu ya vyoo **871** sawa na **38.6%** ya yaliyohitajika. Aidha, Halmashauri ilihitaji nyumba za walimu **1,565** zilizokuwepo **192** na kufanya upungufu wa nyumba za walimu **1,464** sawa na **93.5%**.

2.1.3 Taarifa za Walimu Katika Shule za Msingi za Serikali

Kwa mwaka 2021, Halmashauri ya Wilaya ya Kyela ilikuwa na jumla ya walimu **895** wa Shule za Msingi za Serikali sawa na **57.2%** ya walimu **1,565** waliokuwa wanahitajika. Hivyo, Halmashauri ilikuwa na upungufu wa walimu **670** sawa na **42.8%**.

2.1.4 Elimu Maalumu

Mwaka 2021, Halmashauri ya Wilaya ya Kyela ilikuwa na jumla ya vitengo **05** vya Elimu Maalumu katika Shule za Msingi vikiwa na jumla ya wanafunzi **352** wakiwemo wavulana **189** na wasichana **163** katika aina **sita (6)** za ulemavu:- viziwi (**37**), ulemavu wa akili (**106**), uoni hafifu (**47**), ulemavu wa viungo (**103**), upofu (**03**) na ualbino (**13**)**.**

3.0 ELIMU YA WATU WAZIMA NA ELIMU NJE YA MFUMO RASMI

Kisera kila Shule ya Msingi au Sekondari ni Kituo cha Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi (EWW na ENMRA). Halmashauri ya Wilaya ya Kyela inaratibu program **tatu** za EWW na ENMRA ambazo:- Mpango wa Elimu ya Msingi kwa Walioikosa (MEMKWA), Mpango wa Uwiano Kati ya Elimu ya Watu Wazima na Jamii (MKEJA) na Elimu ya masomo ya kujiendeleza ya Stashahada ya Walimu.

3.1 MEMKWA

Mwaka 2021 Halmashauri imeandikisha jumla ya wanafunzi **102** (wav.**38** na was**.64**) wa MEMKWA sawa na **25.5%** ya matarajio ya kuandikisha wanafunzi **400** (wav.**150** na was.**250**). Wanafunzi hao wangawanywa katika makundirika mawili yaani kundirika la **Kwanza** lenye wanafunzi **90** (wv.**33** na was.**57**) na kundirika la **Pili** lenye wanafunzi **12** (wav.**5** na was.**7**). Wanafunzi hao wanawezeshwa na walimu **18** (Me**.16** na Ke**.2**)**.**

3.2 Elimu ya Kujiendeleza Stashahada ya Walimu

Katika Mwaka 2021, kulikuwa na jumla ya Walimu **174** (Me.**75** na Ke.**99**) wanajiendeleza katika Stashahada ya Ualimu. Walimu hao wanatarajia kuhitimu Stashahada hapo mwezi Disemba, 2022.

4.0 MAENDELEO YA TAALUMA NA HALI YA UFAULU KATIKA SHULE ZA MSINGI

Kuanzia mwaka 2019 matokeo ya Mitihani ya Kitaifa Elimu ya Shule za Msingi yamekuwa yakiboreka. Pamoja na ufaulu kuongezeka katika Mitihani ya Kitaifa bado nafasi ya Halmashauri katika Mitihani hiyo hairidhishi. Ufaulu wa jumla na nafasi ya Halmashauri katika Mitihani ya Upimaji wa kitaifa na Kumaliza Elimu ya Shule za Msingi kuanzia mwaka 2019 ni kama ifuatavyo:-

- Ufaulu wa Upimaji wa Kitaifa Darasa la Nne (SFNA) ulishuka kutoka **96.9%** Mwaka, 2019 hadi **94.6%** Mwaka 2020. Kwa Mwaka 2021, Ufaulu ulipanda kwa **0.9%** hadi **95.5%** na Halmashauri kushika **nafasi ya Kwanza** kimkoa. **Lengo la Mwaka 2022 ni kufikisha Ufaulu wa 100%.**
- Ufaulu wa Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi (PSLE), Mwaka 2019 ulikuwa **86.5%** na Halmashauri ilishika nafasi ya **03** kati ya **07**. Mwaka 2020 kadhalika ufaulu ulishuka kwa **6.3%** hadi **80.2%** ambapo Halmashauri ilishika nafasi ya **04** kimkoa. Mwaka 2021 ufaulu ulipanda kwa **8.4%** hadi **88.6%** hivyo Halmashauri kushika nafasi **03. Lengo la Mwaka 2022 ni kufikisha ufaulu wa 95%.**

4.1 Matokeo ya Upimaji wa Kitaifa Darasa la Nne (SFNA) 2021

4.1.1 Matokeo ya jumla

Jumla ya wanafunzi **7,742** (wav**.3,286** na was**.3,456)** walifanya Upimaji mwaka 2021 ukilinganisha na wanafunzi **7,543** (wav**.3,862** na was**.3,681)** waliofanya Upimaji kama huo mwaka 2020. Aidha, idadi ya wanafunzi waliofanya Upimaji mwaka 2021 iliongezeka kwa wanafunzi **199 (2.6%)** ukilinganisha na wanafunzi waliofanya mwaka 2020.

Jumla ya wanafunzi **6,437** sawa na **95.5%** (wavulana **3,098** sawa na **94.3%** na wasichana **3,339** sawa na **96.6**) walifaulu Upimaji. Ufaulu wa jumla uliongezeka kwa **0.9%** kutoka **94.6%** Mwaka 2020 mpaka **95.5%** Mwaka 2021.

Uchambuzi wa matokeo hayo unaonesha idadi wanafunzi wengi wapo katika **Daraja C** lenye wanafunzi **3,459** sawa na **53.7%**. Aidha, wanafunzi waliofuatia kwa idadi kubwa ni waliofaulu **Daraja D** lenye wanafunzi **1,455** sawa na **22.6%, Daraja B** wanafunzi **1,398** sawa na **21.7%** na **Daraja A** wanafunzi **125** sawa na **1.9%.**

4.1.2 Ulinganifu wa Ufaulu (SFNA) 2020 - 2021 Kimadaraja

Jedwali Na. 2: Ulinganifu wa ufaulu (SFNA) 2020 na 2021 Kimadaraja

Na	DARAJA	UFAULU MADARAJA 2020						UFAULU MADARAJA 2021						TOFAUTI
		IDADI			ASILIMIA			IDADI			ASILIMIA			
		WV	WS	JML	WV	WS	JML	WV	WS	JML	WV	WS	JML	
1	**A**	75	59	**134**	56.0	44.03	1.776	69	56	**125**	55.2	44.8	1.85	**+0.08**
2	**B**	775	588	**1363**	56.9	43.14	18.07	721	677	**1398**	51.57	48.43	20.7	**+2.67**
3	**C**	1703	1738	**3441**	49.5	50.51	45.62	1597	1862	**3459**	46.17	53.83	51.3	**+5.69**
4	**D**	1078	1122	**2200**	49.0	51.00	29.17	711	744	**1455**	48.87	51.13	21.6	**-7.58**
5	**E**	232	173	**405**	57.3	42.72	5.369	188	117	**305**	61.64	38.36	4.52	**-0.85**
JUMLA		**3863**	**3680**	**7543**	51.2	48.79	**100**	**3286**	**3456**	**6742**	48.74	51.26	**100**	**0**

Jedwali linaonesha kwamba; Ufaulu wa SFNA mwaka 2021 kimadaraja uliongezeka kwa kila Daraja ukilinganisha na mwaka 2020. Ongezeko lilikuwa kidogo zaidi katika Daraja la **A** na **C. Aidha, kulikuwa na kupungua kwa idadi ya D na E katika Mwaka huo.**

4.1.3 Ufaulu Kishule Upimaji wa SFNA 2021

Jumla ya shule **104** zilizofanya Upimaji wa Darasa la Nne 2021, Kati ya shule hizo, Shule **moja** sawa na **0.96%** ilipata ufaulu wa **Daraja A,** Shule **5** sawa na **4.8%** zilipata ufaulu wa **Daraja B**, Shule **89**s awa na **85.6%** zilipata ufaulu wa **Daraja C**, na Shule **9** sawa na **8.7%** zilipata ufaulu wa **Daraja D. Hakuna Shule iliyoapata ufaulu wa Daraja la E.**

4.1.3.1 Shule 10 zilizofanya vizuri kwa kigezo cha Wastani

Katika kundi hili Kati ya Shule **10** zilizofanya vizuri zaidi, Shule **02** siyo za serikali na **08** za serikali. Shule **03** zilitoka Tarafa ya Ntebela na Shule **07** kutoka Tarafa ya Unyakyusa.

Jedwali Na. 3: Shule 10 za Kwanza kwa Msingi wa Wastani

Na	TARAFA	SHULE	A-D				E				WASTANI
			Wv	Ws	JML	%	Wv	Ws	JML	%	
1	UNYAKYUSA	KIDZCARE KYELA	9	17	26	100	0	0	0	0	**267.3846**
2	UNYAKYUSA	NYASA ENG. MED.	56	50	106	100	0	0	0	0	**230.9811**
3	UNYAKYUSA	MBALA	33	35	68	100	0	0	0	0	**203.0588**
4	UNYAKYUSA	KEIFO ENG. MED.	6	20	26	100	0	0	0	0	**202.2308**
5	NTEBELA	KYANGALA	11	8	19	100	0	0	0	0	**188.1053**
6	UNYAKYUSA	KATI	83	76	159	100	0	0	0	0	**182.5472**
7	UNYAKYUSA	NDANDALO	48	47	95	98.96	1	0	1	1.042	**175.3750**
8	NTEBELA	MATEMA	88	68	156	99.36	0	1	1	0.637	**170.1529**
9	NTEBELA	MAHENGE	17	22	39	100	0	0	0	0	**168.7179**
10	UNYAKYUSA	IBUNGU	16	15	31	100	0	0	0	0	**167.8710**

Jedwali hapo juu linaonesha kwamba Shule ya Msingi ya **Kidzcare English Medium** ilikuwa ya **Kwanza** kwa ufaulu wa Wastani wa **Alama 267.3846** katika Upimaji wa Kitaifa Darasa la Nne (SFNA) 2021**.** Shule ya Msingi ya **Nyasa English Medium** ilishika nafasi ya **Pili** kwa ufaulu wa Alama **230.9811**. Shule ya Msingi ya Mbala ilikuwa ya **Tatu** kwa ufaulu wa Alama **203.0588.** Shule ya Msingi ya **Keifo English Medium** ilikuwa ya **Nne** kwa ufaulu wa Alama **202.2308.** Shule ya Msingi ya **Kyangala** ilishika nafasi ya **Tano** kwa kupata ufaulu wa Alama **188.1053. Shule nyingine 5 zimeoneshwa katika Jedwali hapo juu.**

4.1.3.2 Shule 10 za Mwisho kwa Msingi wa Ufaulu wa Wastani

Katika shule **10** zilizokuwa na Ufaulu usioridhisha zaidi zilipata wastani wa kuanzia **Alama 121 mpaka 107.** Katika kundi hili Tarafa ya **Unyakyusa** ilikuwa na Shule **03** na Shule **07** zilitoka Tarafa ya **Ntebela**.

Jedwali Na. 4: Shule 10 za Mwisho kwa Msingi wa Wastani

Na	TARAFA	SHULE	A-D				E				WASTANI
			Wv	Ws	JML	%	Wv	Ws	JML	%	
1	NTEBELA	KABULA	4	12	16	100	0	0	0	0	**107.7500**
2	UNYAKYUSA	LUBAGA	35	37	72	80.9	14	3	17	19.1	**111.0337**
3	NTEBELA	TENENDE	20	32	52	88.14	4	3	7	11.86	**111.4407**
4	NTEBELA	IKOMBE	33	44	77	87.5	6	5	11	12.5	**114.1136**
5	NTEBELA	LUTUSYO	10	8	18	94.74	1	0	1	5.263	**114.2105**
6	NTEBELA	MASEBE	17	21	38	92.68	2	1	3	7.317	**114.8780**
7	NTEBELA	MABUNGA	33	43	76	89.41	5	4	9	10.59	**115.9294**
8	UNYAKYUSA	ISANGA	14	16	30	83.33	3	3	6	16.67	**118.6667**
9	UNYAKYUSA	LWANGWA	15	20	35	87.5	3	2	5	12.5	**118.7250**
10	NTEBELA	LUKAMA	14	13	27	96.43	0	1	1	3.571	**121.2143**

Kwa ujumla ufaulu wa Upimaji wa Darasa la Nne (SFNA) 2021 ni mzuri kwa jicho moja ingawa kuna viashiria vya kuzingatia wakati wa kuandaa wanafunzi hawa kuingia Darasa la saba **mwaka 2024** kama ifuatavyo.

i) Idadi kubwa ya wanafunzi (**53.7%)** wamefaulu kwa **Daraja C** ambalo siyo zuri katika ubora wa ufaulu.

ii) Idadi kubwa ya wanafunzi **(22.6%)** waliopata **Daraja D** ni kubwa sana na Daraja hili halihesabiki katika madaraja ya ufaulu katika mtihani wa kuhitimu Elimu ya Msingi (PSLE).

iii) Mtihani wa Upimaji Darasa la Nne ni kipimo cha **KKK** na wanafunzi wanaopata **Daraja D** wengi wao hawamudu Stadi za **KKK.**

5.0 MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI (PSLE) 2021

Halmashauri ya Wilaya ya Kyela ilikuwa na jumla ya wanafunzi **6,253** (wav. **3,017** na was. **3,236**) waliandikishwa Darasa la Saba mwaka 2021. Idadi ya walioandikishwa Darasa la

Saba 2021 ilikuwa sawa na **86.8%** (wav**. 84.8%** na was**.88.7%**) ya wanafunzi **7,207** (wav **3,559** na was **3,648**) walioandikishwa Darasa la Kwanza **mwaka 2015.**

Hii ina maana kwamba wanafunzi **954** (wav**.542** na was**.412**) sawa na **13.2%** (wav.**15.2%** na was**.11.3%**) **hawakufika Darasa la Saba mwaka 2021** kama ilivyotarajiwa kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo utoro. **Inasisitizwa kuwa mamlaka katika ngazi zote zihakikishe utoro unakomeshwa.**

5.1 Matokeo ya PSLE 2021

5.1.1 Matokeo ya Jumla

Jumla ya wanafunzi **5,483** sawa na **88.6%** (wavulana **2678** sawa na **89.9%** na wasichana **2,805** sawa na **87.4%**) walifaulu Mtihani wa Kumaliza Darasa la Saba (PSLE) 2021. Ufaulu wa jumla umeongezeka kwa **8.6%** kutoka **80.2%** Mwaka 2020 mpaka **88.6%** Mwaka 2021.

Uchambuzi wa matokeo hayo unaonesha idadi wanafunzi wengi wapo katika **Daraja C** lenye wanafunzi **4,311** sawa na **78.6%**, **Daraja B** wanafunzi **1112** sawa na **20.3%** na **Daraja A** wanafunzi **60** sawa na **1.09%.** Aidha, wanafunzi **705** sawa na **12.9%** walipata **Daraja D na E.** Katika Mtihani huo, **Ufaulu wa wavulana ni 2.5% zaidi ya wasichana.**

Aidha, Ufaulu wa Daraja la C sio mzuri sana kwa upatikanaji wa Elimu ya Sekondari. Uzoefu unaonesha wengi wa Wanafunzi wanaopata Ufaulu huu hawaripoti shuleni, ama kuchelewa kuripoti, wengine wao huacha Shule (hudondoka) na wengine hufeli Kidato cha Pili na Nne au hupata Daraja 4.

5.1.2 Ulinganifu wa Ufaulu (PSLE) 2020 - 2021 Kimadaraja

Jedwali Na.5: Ulinganifu wa ufaulu (PSLE) 2020 na 2021 Kimadaraja

Na	DA	UFAULU MADARAJA 2020	UFAULU MADARAJA 2021	TO FA UTI

		IDADI			ASILIMIA			IDADI			ASILIMIA			
		WV	**WS**	**JML**	**WV**	**WS**	**JML**	**WV**	**WS**	**JML**	**WV**	**WS**	**JML**	
1	**A**	57	32	**89**	64.04	35.96	1.40	28	32	**60**	46.67	53.33	0.97	**-0.43**
2	**B**	634	419	**1053**	60.21	39.79	16.58	639	473	**1112**	57.46	42.54	17.97	**+1.39**
3	**C**	1841	2113	**3954**	46.56	53.44	62.26	2011	2300	**4311**	46.65	53.35	69.67	**+7.41**
4	**D**	560	660	**1220**	45.90	54.10	19.21	297	404	**701**	42.37	57.63	11.33	**-7.88**
5	**E**	24	11	**35**	68.57	31.43	0.55	3	1	**4**	75.00	25.00	0.06	**-0.49**
JUMLA		**3116**	**3235**	**6351**	**49.06**	**50.94**	**100**	**2978**	**3210**	**6188**	**48.13**	**51.87**	**100**	

Jedwali linaonesha kwamba; Ufaulu wa PSLE mwaka 2021 kimadaraja uliongezeka kwa **Daraja B na C** ukilinganisha na mwaka 2020. **Aidha, kulikuwa na kupungua kwa idadi ya Daraja A, D na E katika Mwaka huo. Matarajio na mipango yetu ni kuhakikisha Daraja D na E zinaendelea kupungua lakini kuzidi kuongeza idadi ya Daraja A, B na C.**

5.1.3 Ufaulu wa Kikata kwa Msingi wa Asilimia

Halmashauri ya Wilaya ya Kyela ina jumla ya kata **33 kati yake Kata 31** ndizo zilizokuwa na watahiniwa wa Darasa la Saba mwaka 2021. Matokeo haya yanaonesha ni Kata **moja tu** ilikuwa na ufaulu wa **Daraja B** sawa na **3.2%,** Kata **30** sawa na **96.8%** zilikuwa na ufaulu wa **Daraja C**. Aidha, katika Mtihani huo, hakuna **Kata hata moja iliyokuwa na** ufaulu **100%.** Kadhalika, **hakuna Kata** iliyokuwa na ufaulu wa chini ya **25%**.

5.1.3.1 Kata 10 za Kwanza kwa Msingi wa Wastani wa Alama.

Katika Mtihani huu, Kata **3** za kwanza zilitoka katika Tarafa ya **Unyakyusa**. **Rejea jedwali Na.6**

Jedwali Na.6: Mpangilio wa Ufaulu kikata, Kata 10 za kwanza kwa Msingi wa Wastani Alama

NA.	JINA LA KATA	WALIOFANYA			WALIOFAULU			ASILIMIA KIKATA 2021	WASTANI KIKATA	DAR AJA
		WAV	WAS	JML	WAV	WAS	JML			
1	KYELA	155	196	351	150	191	341	97.15	198.094	B
2	MWANGANYANGA	137	125	262	134	117	251	95.80	170.733	C
3	ITUNGE	89	107	196	87	105	192	97.96	169.235	C
4	NDANDALO	73	110	183	70	103	173	94.54	168.152	C
5	IKOLO	40	41	81	38	40	78	96.30	165.436	C
6	BONDENI	102	104	206	100	98	198	96.12	162.627	C
7	IPYANA	73	86	159	70	82	152	95.60	162.513	C
8	MUUNGANO	22	36	58	20	33	53	91.38	162.211	C
9	IKIMBA	159	193	352	149	181	330	93.75	159.770	C
10	NGONGA	92	117	209	81	105	186	89.00	157.942	C

5.1.3.2 Kata 10 za Mwisho kwa Msingi wa Wastani wa Alama

Katika Mtihani huo, Kata **10** za Mwisho kwa Msingi wa Wastani wa Alama ni kama zilivyoneshwa katika **Jedwali Na. 7**

Jedwali Na.7: Kata 10 za mwisho kwa Msingi wa Wastani wa Alama

NA.	JINA LA KATA	WALIOFANYA			WALIOFAULU			ASILIMIA KIKATA 2021	WASTANI KIKATA	DARAJA
		WAV	WAS	JML	WAV	WAS	JML			
1	NGANA	104	95	199	92	82	174	87.44	**131.151**	C
2	NKOKWA	44	34	78	27	25	52	66.67	**131.850**	C
3	KISALE	117	131	248	83	98	181	72.98	**135.460**	C
4	TENENDE	69	67	136	48	52	100	73.53	**136.275**	C
5	TALATALA	64	65	129	54	47	101	78.29	**144.002**	C
6	IKAMA	61	45	106	56	32	88	83.02	**146.107**	C
7	KAJUNJUMELE	55	71	126	50	60	110	87.30	**146.383**	C
8	MABABU	156	173	329	135	140	275	83.59	**146.714**	C
9	ITOPE	72	62	134	61	46	107	79.85	**147.075**	C
10	BUJONDE	88	79	167	79	65	144	86.23	**147.978**	C

5.1.4 Matokeo ya PSLE 2021 Kishule

Kama ilivyoelezwa katika utangulizi, Halmashauri ya Wilaya ya Kyela kwa Mwaka 2021 ilikuwa na Shule **107,** kati yake Shule **104 ndizo** zilikuwa na watahiniwa wa Darasa la Saba mwaka 2021.

Uchambuzi ulionesha kuwa, jumla ya shule **13** sawa na **12.5%** zilikuwa na ufaulu wa **100%**. Shule **88 (84.6%)** zilikuwa na ufaulu wa asilimia **50 – 99%**. Shule **02** (**1.9%**) zilikuwa na ufaulu wa **1–49%**. **Shule moja ya NDUKA haikufaulisha kabisa mwanafunzi hata mmoja**. Shule hiyo ilikuwa na jumla ya watahiniwa **06 tu**. **Jedwali hapa Na.8 chini** linaonesha mchanganuo wa makundi hayo.

Jedwali Na. 8 : Idadi ya Shule kimakundi kwa Msingi wa Asilimia

NA	IDADI YA SHULE	ASILIMIA (%)							
		100	%	99-50	%	49-1	%	0	%
2	104	13	12.50	88	84.60	2	1.92	1	0.962

5.1.4.1 Shule 10 za kwanza ushindi wa jumla kwa Msingi wa Wastani

Idadi ya shule kimadaraja ni kama ifuatavyo:- **A= 1 (0.96%); B = 2 (1.9%); C = 98 (94.23%); na D = 2 (1.9%).** Shule **1 (0.96%)** ilipata daraja la **E.**

Shule iliyoongoza kwa Ufaulu wa msingi wastani Mtihani wa Kumaliza Darasa la Saba (PSLE) 2021 ushindi wa jumla ni **Nyasa English Medium** ambayo ilipata jumla ya wastani wa alama **244.619** sawa na **Daraja A**. Katika shule zote **104 zilizokuwa na watahniwa, Nyasa English Medium ilikuwa ni** shule **pekee** yenye ufaulu wa **Daraja A**. Shule nyingine zinazofuatia zimeoneshwa katika **Jedwali Na. 9 hapa chini.**

Jedwali Na. 9: Shule 10 za Kwanza Ushindi wa Jumla kwa Msingi wa Wastani wa Alama

S/N	JINA LA SHULE	WALIOFANYA MTIHANI			UFAULU WA MADARAJA																						
					A			B			C			A-C			WASTANI	%	D			E			D-E			%
		WAV	WAS	JML	WAV	WAS	JML	WAV	WAS	JML	WAV	WAS	JML	WAV	WAS	JML			WAV	WAS	JML	WAV	WAS	JML	WAV	WAS	JML	
1	NYASA ENGL.	34	37	71	19	26	45	15	11	26	0	0	0	34	37	**71**	244.62	100	0	0	0	0	0	0	0	0	**0**	**0**
2	KIDZCARE KYELA	10	19	29	1	1	2	8	16	24	1	2	3	10	19	**29**	207.17	100	0	0	0	0	0	0	0	0	**0**	**0**
3	KYELA	59	73	132	0	0	0	51	47	98	8	26	34	59	73	**132**	193.75	100	0	0	0	0	0	0	0	0	**0**	**0**
4	SEBE	19	12	31	0	0	0	13	1	14	6	11	17	19	12	**31**	177.16	100	0	0	0	0	0	0	0	0	**0**	**0**
5	MWENGE	104	90	194	1	0	1	50	24	74	53	64	117	104	88	**192**	174.34	99	0	2	2	0	0	0	0	2	2	**1.03**
6	NDOLA	11	14	25	1	0	1	6	1	7	4	13	17	11	14	**25**	173.88	100	0	0	0	0	0	0	0	0	0	**0**
7	UHURU	47	42	89	2	1	3	16	16	32	29	23	52	47	40	**87**	173.47	97.8	0	2	2	0	0	0	0	2	2	**2.25**
8	KATI	68	87	155	0	1	1	29	35	64	37	49	86	66	85	**151**	173.45	97.4	2	2	4	0	0	0	2	2	4	**2.58**

9	KEIFO ENGL.	6	7	13	0	0	0	1	2	3	5	5	10	6	7	**13**	173.00	100	0	0	0	0	0	0	0	0	**0**	**0**
10	BUKINGA	14	27	41	0	0	0	11	3	14	2	22	24	13	25	**38**	170.95	92.7	1	2	3	0	0	0	1	2	**3**	**7.32**

5.1.4.2 Shule 10 za Mwisho kwa Msingi wa Wastani wa Alama

Jedwali Na.10: Shule 10 za Mwisho kwa Msingi wa Wastani wa Alama

S/N	JINA LA SHULE	WALIOFANYA MTIHANI			UFAULU WA MADARAJA																								
					A			B			C			A-C			WASTANI	%	D			E			D-E			%
		WAV	WAS	JML	WAV	WAS	JML	WAV	WAS	JML	WAV	WAS	JML	WAV	WAS	JML			WAV	WAS	JML	WAV	WAS	JML	WAV	WAS	JML	
1	NDUKA	3	3	6	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0	**0**	58.833	0	1	2	3	2	1	3	3	3	**6**	**100**
2	KABULA	11	12	23	0	0	0	0	0	0	4	6	10	4	6	**10**	119.174	43	7	6	13	0	0	0	7	6	**13**	**56.5**
3	KANGA	20	25	45	0	0	0	0	0	0	8	11	19	8	11	**19**	121.00	42	12	14	26	0	0	0	12	14	**26**	**57.8**
4	TENENDE	24	26	50	0	0	0	0	0	0	8	18	26	8	18	**26**	125.72	52	16	8	24	0	0	0	16	8	**24**	**48**
5	KANDETE	21	20	41	0	0	0	0	0	0	13	11	24	13	11	**24**	131.17	59	8	9	17	0	0	0	8	9	**17**	**41.5**
6	MWAMBUSYE	16	12	28	0	0	0	3	0	3	8	7	15	11	7	**18**	131.92	64	5	5	10	0	0	0	5	5	**10**	**35.7**
7	KYIJILA	16	10	26	0	0	0	0	0	0	9	9	18	9	9	**18**	131.962	69	7	1	8	0	0	0	7	1	**8**	**30.8**

8	USHIRIKA	13	4	17	0	0	0	0	0	0	9	4	13	9	4	**13**	134.765	76	4	0	4	0	0	0	4	0	**4**	**23.5**
9	LWANGWA	17	9	26	0	0	0	0	0	0	13	6	19	13	6	**19**	134.962	73	4	3	7	0	0	0	4	3	**7**	**26.9**
10	LUSUNGO	23	26	49	0	0	0	2	0	2	16	17	33	18	17	**35**	136.878	71	5	9	14	0	0	0	5	9	**14**	**28.6**

5.1.4.3 Ongezeko la ufaulu Kishule Kwa kigezo cha Wastani wa Alama

Jumla ya Shule **100 (96.2%)** ziliongeza ufaulu wa Wastani wa Alama. Kwa upande mwingine Shule **4 (3.8%)** zilishuka ufaulu wa wastani wa Alama. Shule **10** za kwanza zenye ongezeko kubwa la wastani wa ufaulu wa Alama zimeoneshwa katika **Jendwali Na.11 hapa chini.**

Jedwali Na. 11 : Shule 10 za kwanza kwa ongezeko la ufaulu wa Watani wa Alama

NA.	JINA LA SHULE	WALIOFANYA MTIHANI			WALIOFAULU				ASILIMIA YA UFAULU 2021			ASILIMIA 2020	NAFASI			WASTANI 2020	TOFAUTI YA WASTANI 2021 NA 2020	TOFAUTI YA ASILIMIA 2021 NA 2020
		WV	WS	JM	WV	WS	JM	WASTANI 2021	WIL	MKO	TAIF	TAIF	H/W	MKOA	TAIFA			
1	NGAMANGA	16	11	27	15	11	26	**170.5185**	93.8	100	**96.3**	**48.7**	37	235	5856	**104.7179**	**65.8006**	**47.58**
2	KYELA	59	73	132	59	73	132	**193.7500**	100	100	**100**	**93.6**	10	143	4049	**139.1844**	**54.566**	**6.38**
3	ITUNGE	21	20	41	21	20	41	**165.0244**	100	100	**100**	**71.6**	47	363	8549	**112.9318**	**52.0926**	**28.41**
4	KIDZCARE	10	19	29	10	19	29	**207.1724**	100	100	**100**	**100**	5	26	1817	**156.0000**	**51.1720**	**0.00**
5	KABANGA	14	13	27	14	13	27	**169.8889**	100	100	**100**	**82.1**	26	171	4618	**120.0000**	**49.8890**	**17.86**
6	LUTUSYO	8	9	17	7	8	15	**153.4706**	87.5	88.9	**88.2**	**59.3**	38	239	5904	**103.7407**	**49.7299**	**28.98**
7	MUUNGANO	17	20	37	16	19	35	**163.4865**	94.1	95.0	**94.6**	**69.8**	42	346	8176	**115.5349**	**47.9516**	**24.83**
8	IBUNGU	13	20	33	13	19	32	**165.0000**	96.9	97.0	**97.0**	**84.4**	28	173	4772	**119.4063**	**45.5940**	**12.59**
9	BUKINGA	14	27	41	13	25	38	**170.9512**	92.7	92.7	**93.0**	**83.7**	21	256	6420	**125.7143**	**45.2370**	**9.01**
10	TALATALA	28	32	60	26	17	43	**139.4167**	71.7	71.6	**72.0**	**47.4**	65	442	10062	**95.8596**	**43.5570**	**24.30**

5.1.4.4 Shule 10 za mwisho kwa ongezeko la ufaulu wa Wastani wa Alama

Shule **10** za mwisho kwa ongezeko la ufaulu kwa kigezo cha Wastani wa Ufaulu zimeoneshwa katika **Jedwali Na.13 hapa chini.**

Jedwali Na.13: Shule 10 za Mwisho kwa ongezeko la Ufaulu Wastani wa Alama

NA.	JINA LA SHULE	WALIOFANYA MTIHANI			WALIOFAULU				ASILIMIA YA UFAULU 2021			ASILIMIA 2020	NAFASI			WASTANI 2020	TOFAUTI YA WASTANI 2021 NA 2020	TOFAUTI YA ASILIMIA 2021 NA 2020
		WAV	WAS	JML	WAV	WAS	JML	WASTANI 2021	WIL	MK	TAIF	TAIF	H/W	MKOA	TAIFA			
1	NDUKA	3	3	6	0	0	0	**58.8333**	0.0	0.0	**0.0**	**40.0**	39	248	6109	**99.4000**	**-40.5667**	**-40.00**
2	USHIRIKA	13	4	17	9	4	13	**134.7647**	69.2	100	**76.5**	**100.0**	4	21	1520	**161.625**	**-26.8603**	**-23.53**
3	NDOBO	15	27	42	15	21	36	**144.1429**	100.0	77.8	**85.7**	**100.0**	2	19	1402	**164.3913**	**-20.2484**	**-14.29**
4	KABULA	11	12	23	4	6	10	**119.1739**	36.4	50.0	**43.5**	**100**	9	77	3263	**135.875**	**-16.7011**	**-56.52**
5	JITEGEMEE	24	32	56	24	28	52	**154.0179**	92.86	90.0	**93.0**	**100**	2	56	2274	**153.1373**	**5.3710**	**-3.22**
6	MBULA	18	25	43	18	23	41	**148.4186**	95.35	96.0	**95.4**	**100**	7	51	2678	**142.4167**	**6.0020**	**-4.65**
7	TENENDE	24	26	50	8	18	26	**125.7200**	33.3	69.2	**52.0**	**85.7**	36	318	7637	**118.8393**	**6.8807**	**-33.71**
8	KEIFO	6	7	13	6	7	13	**173.0000**	100	100	**100**	**100**	1	16	362	**165.2667**	**7.7330**	**0.00**
9	MWAMBUSYE	16	12	28	11	7	18	**131.9286**	68.8	58.3	**64.3**	**85.0**	23	156	4493	**122.7000**	**9.2286**	**-20.71**

10	IKULU	28	30	58	25	30	55	**162.5862**	94.97	95.0	**94.9**	**100**	2	56	2274	**153.1373**	**9.4490**	**-5.17**

5.1.5 Matokeo kimasomo kwa Msingi wa Asilimia PSLE 2021

Kihalmashauri, somo la **Kiswahili** ndilo **lililofanywa vizuri zaidi** (**95.83%).** Ufaulu wa masomo mengine umeoneshwa katika mabano kama ifuatavyo:- **Sayansi (87.62%), Uraia na Maadili (84.24%), M/Jamii (73.79%**), **Hisabati (57.24%) na English (36.4%).** Ufaulu wa Masomo kwa msingi wa Asilimia Kimadaraja umeoneshwa katika **Jedwali Na. 14 hapa chini.**

Jedwali. Na.14: Matokeo ya PSLE 2021 Kimasomo na Kimadaraja

SOMO	WALIOFANYA			MATOKEO YA MASOMO KIMADARAJA																		
				A			B			C			A-C				D			E		
	WV	WS	JML	WV	WS	JML	WV	WS	JML	WV	WS	JML	WV	WS	JML	%	WV	WS	JML	WV	WS	JML
Kiswahili	2978	3209	6187	681	726	1407	1531	1708	3239	633	650	1283	2845	3084	5929	**95.83**	113	112	225	22	11	33
Hisabati	2978	3210	6188	41	27	68	326	194	520	1495	1459	2954	1862	1680	3542	**57.24**	1093	1506	2599	23	24	47
English	2978	3209	6187	59	58	117	129	133	262	903	970	1873	1091	1161	2252	**36.40**	1847	2024	3871	40	24	64
Sayansi	2978	3210	6188	129	49	178	1148	873	2021	1432	1791	3223	2709	2713	5422	**87.62**	253	489	742	16	8	24
M/Jamii	2978	3210	6188	26	12	38	624	337	961	1667	1900	3567	2317	2249	4566	**73.79**	653	951	1604	8	10	18
Maadili	2978	3210	6188	2	0	2	694	669	1363	1849	1999	3848	2545	2668	5213	**84.24**	398	504	902	35	38	73

5.1.6 Ufaulu wa Wanafunzi PSLE 2021

Uchambuzi wa Matokeo unaonesha kuwa mwanafunzi aliyeongoza kwa Ufaulu wa jumla ni **ULLY ISACK MWAMBULO (mvulana)** kutoka Shule ya Msingi **Nyasa English Medium** mwenye jumla ya ufaulu wa **alama 268 (A)** ana **A katika masomo 5 na B moja.**

Mwanafunzi aliyeshika nafasi ya **Pili** anaitwa **NANCY FRIDAY MBWILE (sichana)** wa anatoka **Nyasa English Medium** alikuwa na ufaulu wa alama **267(A)** ana **A katika masomo 5 na B moja.**

5.1.6.1 Wanafunzi 10 waliongoza Ushindi wa Jumla

Wanafunzi **10** wa kwanza wote walitoka katika shule **moja ya Nyasa English Medium**. Aidha, katika kundi hili, **wavulana ni watatu na wasichana ni saba**.

Jedwali Na .15: Wanafunzi 10 wa Kwanza Ushindi wa Jumla

Na.	SHULE YA MSINGI ALIYOTOKA	PREM NAMBA	NAMBA YA MTAHINIWA	JINSI	JINA LA MWANAFUNZI	MKOA	WILAYA	JML
1	NYASA ENG. MEDIUM	20150175301	PS10031010034	ME	ULLY ISACK MWAMBULO	MBEYA	KYELA	**268**
2	NYASA ENG. MEDIUM	20151339721	PS10031010065	KE	NANCY FRIDAY MBWILE	MBEYA	KYELA	**267**
3	NYASA ENG. MEDIUM	20151078589	PS10031010055	KE	KISSAH DICKSON MWANKANDA	MBEYA	KYELA	**266**
4	NYASA ENG. MEDIUM	20153461076	PS10031010067	KE	SEKELA WILLIAM MWAKALAMBILE	MBEYA	KYELA	**266**
5	NYASA ENG. MEDIUM	20151078557	PS10031010020	ME	JUNIOR ANDREW NKOMOLA	MBEYA	KYELA	**264**
6	NYASA ENG. MEDIUM	20151078585	PS10031010051	KE	HERNESTA AMOSI KYEJO	MBEYA	KYELA	**264**
7	NYASA ENG. MEDIUM	20151210777	PS10031010052	KE	IREEN BENEDICT NDOSA	MBEYA	KYELA	**263**
8	NYASA ENG. MEDIUM	20151078591	PS10031010057	KE	LEAH NSAJIGWA MWAKAPALALA	MBEYA	KYELA	**263**
9	NYASA ENG. MEDIUM	20151078586	PS10031010053	KE	JACKLINE AUGUSTINO KYANDO	MBEYA	KYELA	**262**
10	NYASA ENG. MEDIUM	20151078550	PS10031010013	ME	HENRY HERRY MHAGAMA	MBEYA	KYELA	**261**

5.1.6.2 Wavulana 10 wa kwanza ushindi wa jumla.

Wanafunzi **10** wa kwanza wavulana walitoka shule za **Nyasa English Medium (8), Maendeleo (1) na Mwenge (1).**

Jedwali Na. 16: Wanafunzi 10 wa Kwanza Ushindi wa Jumla Wavulana

Na.	SHULE YA MSINGI ALIYOTOKA	PREM NAMBA	NAMBA YA MTAHINIWA	JINSI	JINA LA MWANAFUNZI	MKOA	WILA YA	JML
1	NYASA ENG. MEDIUM	20150175301	PS10031010034	ME	ULLY ISACK MWAMBULO	MBEYA	KYELA	**268**
2	NYASA ENG. MEDIUM	20151078557	PS10031010020	ME	JUNIOR ANDREW NKOMOLA	MBEYA	KYELA	**264**
3	NYASA ENG. MEDIUM	20151078550	PS10031010013	ME	HENRY HERRY MHAGAMA	MBEYA	KYELA	**261**
4	NYASA ENG. MEDIUM	20151078555	PS10031010018	ME	JOSHUA MNYIKA SPEAR	MBEYA	KYELA	**259**
5	NYASA ENG. MEDIUM	20151078548	PS10031010011	ME	GODLBLESS KASYUPA ANYITIKE	MBEYA	KYELA	**257**
6	MAENDELEO	20151142904	PS10030560014	ME	DANIEL NETTO MWATWABANA	MBEYA	KYELA	**256**
7	NYASA ENG. MEDIUM	20151078561	PS10031010024	ME	LUSAJO AMANI MWAKIPESILE	MBEYA	KYELA	**256**
8	NYASA ENG. MEDIUM	20151210768	PS10031010033	ME	TWANDILE IPYANA MWANGOSI	MBEYA	KYELA	**254**
9	MWENGE	20151140822	PS10030770071	ME	MATHIAS THOBIAS MOLLINGA	MBEYA	KYELA	**253**
10	NYASA ENG. MEDIUM	20151078552	PS10031010015	ME	JESSE JOSEPH MWAKIJELE	MBEYA	KYELA	**253**

5.1.6.3 Wanafunzi 10 wa kwanza wasichana ushindi wa jumla

Wanafunzi wasichana **10** walioongoza wote walitoka Shule **ya Nyasa English Medium**

Jedwali Na. 17: Wanafunzi 10 wa Kwanza Ushindi wa Jumla Wasichana

Na.	SHULE YA MSINGI ALIYOTOKA	PREM NAMBA	NAMBA YA MTAHINIWA	JINSI	JINA LA MWANAFUNZI	MKOA	WILAYA	JML
1	NYASA ENG. MEDIUM	20151339721	PS10031010065	KE	NANCY FRIDAY MBWILE	MBEYA	KYELA	**267**
2	NYASA ENG. MEDIUM	20151078589	PS10031010055	KE	KISSAH DICKSON MWANKANDA	MBEYA	KYELA	**266**
3	NYASA ENG. MEDIUM	20153461076	PS10031010067	KE	SEKELA WILLIAM MWAKALAMBILE	MBEYA	KYELA	**266**
4	NYASA ENG. MEDIUM	20151078585	PS10031010051	KE	HERNESTA AMOSI KYEJO	MBEYA	KYELA	**264**
5	NYASA ENG. MEDIUM	20151210777	PS10031010052	KE	IREEN BENEDICT NDOSA	MBEYA	KYELA	**263**
6	NYASA ENG. MEDIUM	20151078591	PS10031010057	KE	LEAH NSAJIGWA MWAKAPALALA	MBEYA	KYELA	**263**
7	NYASA ENG. MEDIUM	20151078586	PS10031010053	KE	JACKLINE AUGUSTINO KYANDO	MBEYA	KYELA	**262**
8	NYASA ENG. MEDIUM	20151078592	PS10031010058	KE	LEAH RICHARD MANUNGWA	MBEYA	KYELA	**261**
9	NYASA ENG. MEDIUM	20151078593	PS10031010059	KE	LETCIA LWITIKO MWAKIPESILE	MBEYA	KYELA	**261**
10	NYASA ENG. MEDIUM	20151078599	PS10031010069	KE	SUBILAGA EDWARD NKYANDWALE	MBEYA	KYELA	**260**

6.0 MAPOKEZI YA FEDHA ZA UENDESHAJI WA SHULE NA MIRADI YA MAENDELEO YA ELIMU KATIKA SHULE ZA MSINGI

Kipindi cha Mwaka 2020/2021 Halmashauri ya Wilaya ya Kyela ilipokea jumla ya kiasi cha **Sh.1,237,495,945.76** kwa ajili ya uendeshaji wa Shule na kutekeleza miradi mbalimbali ya Maendeleo ya Elimu katika Shule za Msingi. **Rejea Jedwali Na.18 hapa chini.**

Jedwali Na.18: Fedha za Miradi ya Maendeleo zilizopokelewa 2020/2021

Na	Aina ya Mradi	Kiasi Kilichopokelewa
1	Elimu Bila Malipo Shule za Msingi (Ruzuku)	651,203,945.76
2	Ujenzi Madarasa mapya (EP4R) Shule za Msingi	200,000,000.00
3	Umaliziaji wa Ujenzi wa Madarasa (EP4R)	125,000,000.00
4	Ujenzi wa Matundu ya vyoo Shule za Msingi (EP4R)	26,400,000.00
5	Uimarishaji wa KKK (UNICEF)	107,092,000.00
6	Maboma ya Nyumba za Walimu (Serikali Kuu)	75,000,000.00
7	Ujenzi wa matundu ya vyoo (COVID-19)	52,800,000.00
JUMLA		**1,237,495,945.76**

6.1 Fedha za Elimu bila Malipo 2020/2021

Kwa kipindi cha mwaka 2020/2021 Halmashauri ilipokea kiasi cha **Sh.651,203,945.76** k upitia fedha za Ruzuku na Elimumsingi Bila Malipo. Fedha hiyo imekuwa na manufaa m akubwa kwa Halmashauri yetu, kwani fedha hiyo imetumika katika maeneo mbalimbali k wa minajili ya uendeshaji wa Shule.

6.2 Fedha za EP4R Ujenzi wa Miundombinu mipya

Mwaka 2020/2021 Halmashauri ilipokea jumla **Sh. 404,200,000.00** kupitia Program ya **Lipa Kulingana na Matokeo (EP4R), na jumla ya Sh. 75,000,000.00 kutoka Serikali kuu** kwa ajili ya ujenzi wa Miundombinu mbalimbali katika Shule za Msingi. Kutokana na fedha hiyo, jumla ya vyumba vya madarasa **21**, matundu ya vyoo **72** na nyumba **3** za Walimu ilijengwa. Miundombinu yote ilikamilka na inatumika. Ujenzi wa miundombinu hiyo umesaidia sana kupunguza uhaba wa madarasa na matundu ya vyoo uliyopo katika shule za Msingi husika. Aidha, umeboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia.

6.3 Fedha za Uimarishaji wa Stadi za KKK kupitia UNICEF

Kwa kipindi cha mwaka 2020/2021, Halmashauri ilipokea jumla ya **Sh.107,092,000.00** kupitia Shirika la **UNICEF Tanzania**. Fedha hizo zilikuwa kwa ajili ya kuendesha mafunzo ya kuongeza umahiri wa ushauri nasaha na unasihi pamoja na SARA REDIO. Mafunzo hayo yaliendeshwa kwa mafanikio na ufanisi mkubwa. Walimu **244** walinufaika kwa kuongeza ujuzi na hivyo kuboresha ufundishaji na Makuzi ya Malezi ya wanafunzi.

7.0 MAFANIKIO

Kwa kipindi cha mwaka 2020/2021 Idara ya Elimu ya Msingi ilipata mafanikio mengi, baadhi ya mafanikio hayo ni kama yafuatayo:-

1. Kuongeza kwa ufaulu kwa **8.6%** katika mitihani ya Taifa Darasa la Saba (PSLE) kutoka **80.2%** hadi **88.6%** na Darasa la Nne (SFNA) kutoka **94.6%** hadi **95.5%.** Hii ni pamoja na ubora wa ufaulu.
2. Kupata jumla ya Walimu **15 Ajira mpya,** wakiwemo wanaume **10** wanawake **5.**
3. Kuendesha mafunzo kwa walimu **244** ya kujenga umahiri katika Makuzi na Malezi ya wanafunzi.
4. Kupandishwa vyeo na kuthibitishwa kazini walimu **239.**
5. Kuongezeka kwa miundombinu katika shule za Msingi. Jumla ya vyumba vya madarasa **21** nyumba za walimu **3** na matundu ya vyoo **72.**
6. Kushika nafasi ya pili Kimkoa ya mashindano ya **UMITASHUMTA** na kupeleka jumla ya wanamichezo **18** ngazi ya Taifa.
7. Kufanya ufuatiliaji katika shule **40** zilizokuwa na ufaulu usioridhisha katika SFNA/PSLE 2020.
8. Ujenzi wa Shule Mpya ya Mchepuo wa Kiingereza ya Njisi (**Mpakani English Medium)** na Usajili wa Shule **5** mpya, zikiwemo Shule **3** za **Ibale, Bagamoyo** na **Bujesi** na Shule **2** zisizo za Serikali za **Think Big English Medium** na **CBMIKU English Medium**.

8.0. CHANGAMOTO NA UTATUZI WAKE

1. **Upungufu mkubwa wa miundombinu Shule za Msingi**. Serikali inaendelea kutoa Fedha za Ujenzi wa Miundombinu kwa kushirikiana na wananchi, wadau wa maendeleo ya Elimu.
2. **Baadhi ya Shule kutotoa chakula cha Mchana.** Jumla ya Shule **66** zinatoa Chakulana Shule **45** hazitoi. Kuendelea kuhimiza na kuelimisha jamii kuchangia chakula cha mchana ni wajibu wa jamii kushirikiana na Wadau.
3. **Upungufu mkubwa wa walimu**. Kwa mwaka 2021, Halmashauri ilikuwa na upungufu wa jumla ya walimu **670.** Pamoja na Serikali kutoa Ajira Mpya ya Walimu, mamlaka husika tunaendelee kushirikisha wadau kutafuta Walimu wa kujitolea. Mpaka sasa Halmashauri ina jumla ya walimu **140** wa kujitolea katika Shule mbalimbali.
4. **Udhaifu wa kimenejimenti katika baadhi ya Shule**. Tunaendelea kupitia menejimenti za Shule zilizopo ili kufanya mabadiliko kwa ajili ya uboreshaji wa utawala na baadae kuinua Taaluma.
5. **Utoro mkubwa wa kudumu na wa rejareja** wa walimu na wanafunzi. Kusimamia mikakati ya kudhibiti utoro ikiwa pamoja na kuwachukulia hatua watoro na wanaosababisha.
6. **Baadhi ya kata kutokuwa na Shule za Msingi za Serikali**. Kata ya **Serengeti** na **Mikoroshini** hazina Shule za Msingi za serikali. Inahimizwa wananchi wahimizwe kujenga shule ili kuharakisha utoaji wa elimu katika maeneo yao.
7. **Baadhi ya Shule za Msingi zimekuwa kubwa** mno (kwa idadi ya wanafunzi). Lubele (**2,000**), Mwenge (**1,748**), Mababu (**1,477**) na Kati (**1,330**). Kusababisha ufundishaji kuwa mgumu. Baadhi ya Shule hizo na nyingine hasa za mjini zinakosa maeneo ya upanuzi/ujenzi wa madarasa. Tunakusudia kuanza kujenga madarasa ya ghorofa.

9.0 MIKAKATI MBALIMBALI YA KUBORESHA TAALUMA NA KUINUA UFAULU

1. Kusimamia na kupima utekelezaji wa **Mikakati 13 ya Wilaya na 10 ya Mkoa** ya kuboresha Taaluma na kuinua ufaulu.
2. Kuhamasisha jamii ili kushiriki kikamilifu kuendelea kujenga miundombinu.

3. Kuendelea kushirikiana na Wadau pamoja na jamii kujenga Shule mpya ili kupunguza msongamano wa wanafunzi lakini pia kuharakisha maendeleo ya Elimu ya Msingi.
4. Kuimarisha ufuatiliaji wa Ufundishaji na Ujifunzaji darasani na kuchukuwa hatua kwa asiyewajibika kikamilifu.
5. Kubuni na kuendesha mafunzo ya ndani kwa walimu ili kuwajengea umahiri.
6. Kudhibiti utoro wa aina zote kwa Walimu na wanafunzi.
7. Kuwasimamia Maafisa Elimu Kata na kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa utendaji kazi wao kila baada ya **miezi mitatu**.
8. Kuhakikisha kila Shule inatoa chakula cha mchana.
9. Kutafuta walimu wa kujitolea kwa Shule zenye upungufu mkubwa wa Walimu.
10. Kufanya ziara za kukutana na walimu ili kuhimiza uwajibikaji na kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabiri.
11. Kurekebisha Ikama ya Walimu kuanzia ngazi ya Kata.

10.0 MWISHO.

Tunapenda kuchukua fursa hii kuwapongeza sana Wadau wetu wote wa Elimu kwa kazi kubwa mnayofanya katika **Kuboresha Taaluma na Kuinua Ufaulu**. Kipekee tunamshukuru sana Mdau wetu mkubwa **COCOA FOR SCHOOLS (CFS)** kwa moyo wake uliotukuka wa kusaidia ujenzi wa Madarasa na kutoa Vifaa mbalimbali vya Kufundishia na Kujifunzia.

Sisi pamoja na Mkoa wa Mbeya Kwa Ujumla, Tunaamini kwamba kila mmoja wetu akiwajibika katika eneo lake kwa Kaulimbiu yetu kwamba, "**KILA MMOJA ANG'ANG'ANE NA KUMUDU KIPANDE CHAKE", Kwa Kufanya Kazi kwa bidii na Kutimiza Wajibu wake Ipasavyo Kwa Ufanisi na Kwa Wakati** – **HALITAKUWEPO JAMBO LOLOTE LITAKALOSHINDIKANA;** Hivyo Wilaya yetu na Mkoa kwa Ujumla Utasonga mbele Kitaaluma!

IMEANDALIWA NA IDARA YA ELIMU YA MSINGI
HALMASHAURI YA WILAYA YA KYELA
JUNI, 2022